# Jarida la eGA Mamlaka ya Serikali Mtandao

Toleo la 12 | Aprili - Juni 2025

# Waziri Mkuu azindua Mfumo wa GovESB




- Azitaka taasisi ambazo bado hazijaunganishwa kufanya hivo kabla ya **Julai 30 2025**

**MAKALA**
e-GA ilivyotekeleza Ilani ya CCM 2020 – 2025 Uk.15

**AFYA**
Wanawake Wapo Katika Hatari Zaidi Ya Kupata Uchakavu Wa Mifupa Uk.9

**UBUNIFU**
Mfumo wa Kufuatilia Kiwango cha Gesi Kidijitali Uk.14

"Karibu tujenge Serikali Kidijitali"

# Yaliyomo


**Tahariri**
Mfumo wa e-Mrejesho : Daraja la Kidijiti kati ya Serikali na Wananchi **Uk. iii**

**Dira yetu**
Usalama wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini ni kipaumbele chetu **Uk.iv**

**Nukuu**
Nukuu kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao **Uk.v**

**Habari**
Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa azindua Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini **Uk. 1-2**

**Habari**
Mfumo wa e-Mrejesho V2 waipeperusha Bendera ya Tanzania Kimataifa **Uk 3**

**Habari**
Hoja za TEHAMA Ripoti ya CAG zifanyiwe kazi **Uk.4**

**Habari**
Waziri Simbachawene aipongeza Bodi ya Wakurugenzi ya e-GA **Uk.5**

**Habari**
Wachambuzi wa Mifumo waaswa kuongeza Weledi na Ufanisi **Uk.6**

**Habari**
Maafisa Habari watakiwa kulinda Taarifa za Serikali **Uk.8**

**Afya**
Wanawake wapo katika hatari zaidi ya kupata uchakavu wa Mifupa **Uk.9-11**

**Vijana na TEHAMA**
Herieth Daudi: Ndoto hai katika kesho ya TEHAMA **Uk.12**

**Wasemavyo Wadau**
**Uk.13**

**Ubunifu**
Mfumo wa kufuatilia kiwango cha Gesi Kidijiti **Uk.14**

**Makala**
e-GA yataja Mafanikio ya Ilani ya CCM 2020 - 2025 **Uk.15-16**

**Matukio katika Picha**
**Uk.17-20**




# Mfumo wa e-Mrejesho : Daraja la kidijiti kati ya Serikali na Wananchi

Katika zama hizi za utawala wa kidijiti, mifumo ya TEHAMA ni nguzo muhimu katika kuboresha huduma za umma. Ipo mifumo mingi inayotumika ndani ya Serikali lakini, kwa leo nitazungumzia Mfumo wa e-Mrejesho.

Mfumo huu umejengwa na kusanifiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mfumo wa eMrejesho unalenga kurahisisha mawasiliano kati ya wananchi na taasisi za serikali, na umejizatiti kuwa chombo cha uwazi na uwajibikaji serikalini.

Aidha, Mfumo huu unawawezesha wananchi kuwasilisha kero, maoni, maswali, mapendekezo, au pongezi kwa taasisi za serikali kwa njia ya kidijitali. Wananchi wanaweza kufuatilia utekelezaji wa malalamiko yao kwa kutumia dashibodi maalum inayowezesha viongozi wa serikali kuona mwenendo wa utekelezaji wa kero na maoni yaliyopokelewa katika taasisi husika.

Ujenzi wa Mfumo huu umezingatia usalama na usiri mkubwa wa taarifa, Wananchi wanapowasilisha maoni au malalamiko yao, mfumo unampa nafasi ya kuchagua kujulikana au kutojulikana kwa kuandika au kutoandika taarifa zake binafsi. Hii inahakikisha faragha na usiri wa taarifa zao.

Aidha, mfumo huu unaziunganisha taasisi zote za Serikali, hivyo taasisi kwa taasisi zinaweza kubadilishana taarifa za malalamiko au maoni yanayotolewa na wananchi. Serikali pia inaweza kupata takwimu za malalamiko hayo, jambo linalosaidia katika kuboresha huduma za umma. Mfumo wa e-Mrejesho umeleta mafanikio makubwa katika kuboresha mawasiliano kati ya Serikali na wananchi. Mnamo mwaka 2024, mfumo huu ulishinda tuzo ya Umoja wa Mataifa kwa ubunifu katika huduma za umma, kutokana na mchango wake katika kukuza uwazi na uwajibikaji katika utawala wa umma kupitia teknolojia.

Vilevile, mwaka huu wa 2025 Mfumo wa e-Mrejesho toleo la pili (e-Mrejesho V2) umeingia hatua ya fainali katika kipengele cha Serikali Mtandao, kwenye Tuzo za Mkutano wa Dunia wa Jumuiya ya TEHAMA mwaka 2025 (World Summit on the Information Society -WSIS 2025 Grand Winner).

Mfumo wa e-Mrejesho ni mfano mzuri wa jinsi teknolojia inavyoweza kutumika kuboresha huduma za umma na kuimarisha uhusiano kati ya serikali na wananchi. Ni muhimu kwa wananchi na taasisi za umma kuendelea kutumia na kuhamasisha matumizi ya mfumo huu ili kufikia malengo ya Serikali Mtandao.

Unaweza kutumia mfumo huu kwa njia zifuatazo; -

1. Kupitia simu ya mkononi kwa kubofya *152*00# na kuchagua namba 8 kisha namba 2.

2. Kupitia tovuti rasmi ya emrejesho.gov.go.tz.

3. Kupitia programu ya simu (mobile app) inayopatikana kwenye Google Play Store na Apple App Store.

4. Kwa pamoja tuiambie Serikali Kidijitali.



**Bi. Subira Kaswaga**
**Meneja Mawasiliano e-GA**

# Usalama Wa Mifumo Ya **TEHAMA Serikalini** Ni Kipaumbele Chetu



Mhandisi Benedict Ndomba
**Mkurugenzi Mkuu e-GA**

Katika zama hizi za maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, usalama wa mifumo ya TEHAMA Serikalini ni kiungo muhimu katika kulinda taarifa za taifa letu. Taarifa ni rasilimali yenye thamani kubwa; ikiwa zitadukuliwa au kupatikana kwa njia zisizo halali, usalama na uthabiti wa taifa unaweza kudidimia.

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ina jukumu muhimu la kusimamia na kudhibiti usalama wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA serikalini. e-GA hutekeleza jukumu hili kwa njia mbalimbili ikiwemo kushirikiana na wadau wa masuala ya usalama wa wa mtandaoni, ili kubaini na kudhibiti matishio ya usalama mtandaoni kabla hayajaleta madhara.

Pili ni utoaji wa mafunzo ya mara kwa mara kwa wataalamu wa TEHAMA ambayo, hulenga kuwajengea uwezo wataalamu katika kubaini na kudhibiti matishio ya kiusalama kwa kutumia teknolojia sahihi. Kwa kuwa teknolojia hubadilika kila mara, ni muhimu kwa wataalamu kuwa na ujuzi wa kisasa ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza.

Tatu ni ujenzi wa Mfumo wa Usalama wa Kidijiti wa NGAO. e-GA imetengeneza Mfumo wa Usalama wa Kidijitali wa Uthibitishaji wa vipengele vingi 'multifactor authentication' ujulikanao kama NGAO.

Mfumo huu unatumia programu ya '**NGAO Authenticator**' inayotengeneza nenosiri la mara moja (**One-Time Password - OTP)** kwa kila uthibitisho wa mtumiaji, hivyo kuongeza usalama wa ziada wa taarifa muhimu kwa watumiaji wa mifumo ya Serikali.

Nne ni uhifadhi wa Taarifa za Serikali katika Maeneo Salama. e-GA inahakikisha kuwa, taarifa za Serikali zinahifadhiwa katika maeneo salama yaliyoidhinishwa, ili kulinda usiri na usalama wa taarifa hizo. Hii ni pamoja na kutumia wataalamu wa ndani katika ujenzi na usanifu wa mifumo ya TEHAMA, ili kupunguza hatari za uvujaji wa taarifa kwa watu wasiohusika.

Nitumie nafasi hii pia, kuzikumbusha taasisi zote za umma kuhakikisha zinahifadhi data zao katika maeneo salama yaliyoidhinishwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao.

Tano, kusimamaia utekelezaji wa Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao. Sheria hizi zinasaidia katika kudhibiti matumizi mabaya ya mifumo ya TEHAMA na kuhakikisha kuwa mifumo inasimamiwa kwa ufanisi na uadilifu wa kutosha.

Nihitimishe kwa kusema kuwa, usalama wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA serikalini ni jukumu letu sote. Kila mtumishi wa umma anayetumia mifumo ya TEHAMA anawajibika katika kulinda usalama wa mifumo hiyo.

Ni wajibu wa kila taasisi ya umma kuwajengea uwezo watumishi wake wote kuhusu usalama wa mtandaoni na namna ambavyo kila mmoja anawajibika katika hili.

# Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao



"Ili tufikie malengo ya kuwa na Serikali Mtandao imara na yenye tija, jitihada za pamoja zinahitajika kwa wadau wote wa Serikali Mtandao, kwa kuhakikisha wanazingatia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika ujenzi na usimamizi wa miradi na mifumo ya TEHAMA Serikalini."

**Dkt. Mussa Kissaka**
**Mwenyekiti wa Bodi**

# Waziri Mkuu azindua Mfumo wa GovESB

Na Ben Bago

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), ameziagiza taasisi za umma, ambazo bado hazijajiunga na Mfumo wa Kuwasiliana na Kubadilishana Taarifa Serikalini **(Government Enterprise Service Bus - GovESB)**, kujiunga na Mfumo huo ifikapo Julai 30, mwaka huu.

Mhe. Majaliwa ametoa agizo hilo Juni 23, wakati akiwasilisha hotuba kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, yaliyofanyika katika viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.

Alisema kuwa, ni lazima taasisi zote za umma zinazotakiwa kujiunga katika mfumo wa GoVESB kufanya hivyo kabla ya tarehe 30 Julai, 2025 ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia katika kurahisisha upatikanaji wa huduma za Serikali kwa wananchi kidijitali.

**"Ni muhimu kujiunga na Mfumo wa GovESB, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia alielekeza kuwa, pindi Mamlaka ya Serikali Mtandao itakapokamilisha ujenzi wa Mfumo huu kila taasisi ihakikishe Mifumo yake inabadilishana taarifa na Mifumo ya taasisi nyingine kupitia Mfumo wa GovESB. Idadi ya taasisi zilizounganishwa hadi sasa ni chache sana ukilinganisha na taasisi za Serikali tulizonazo"**

**Mhe. Kassim Majaliwa**
**Waziri Mkuu**

Aliongeza kuwa, taasisi zote za umma zinapaswa kujiunga na Mfumo huo kwani, licha ya kuwa na faida nyingi zinazochagiza kuongezeka kwa ufanisi ndani ya Serikali na kuwezesha utoaji wa huduma bora za Serikali kwa wananchi kwa wakati, lakini pia hauna gharama.

"Hakuna sababu ya taasisi yeyote kutounganishwa na Mfumo huu, na muda ukifika nitaomba nipatiwe taarifa ya utekelezaji, na taasisi ambazo zitakuwa bado hazijajiunga na Mfumo huu zitakuwa ndiyo zinakula rushwa", alisema Mhe. Majaliwa.






Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwaakizungumza wakati wa uzinduzi wa Mfumo wa Ubadilishanaji taarifa (GoVESB)

mbalimbali ya TEHAMA Serikalini, jambo ambalo linachangia kukuza vipaji vya wazawa na pia kuongeza usalama wa Mifumo na taarifa za Serikali.

Alisema kuwa, ni muhimu kuwapongeza vijana wote wa kitanzania wanaoshiriki katika ujenzi wa Mifumo mbalimbali ya TEHAMA ndani ya Serikali ili kuwapa moyo wa kuendelea kufanya kazi kwa bidii zaidi.

Sambamba na hayo, Mhe. Majaliwa alitoa tuzo kwa Maafisa TEHAMA 15 wa e-GA walioshiriki kutengeneza Mfumo wa GoVESB na kuwasihi kuendelea kufanya vizuri zaidi katika ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi-Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene (Mb) alisema, matumizi ya Mfumo wa GovESB yamepunguza urasimu na msongamano katika ofisi za umma, ambazo hubadilishana taarifa kupitia Mfumo huo.

"Ubadilishanaji wa taarifa kupitia mfumo huu unaharakisha sana utoaji wa huduma kwa sababu watoa huduma wote wanasomana hivyo inampunguzia adha mwananchi ya kutembea kutoka ofisi moja hadi nyingine ili kupata huduma", alifafanua Mhe. Simbachawene.

Tangu kuanza kutumika rasmi kwa Mfumo wa GoVESB, taasisi za umma zaidi ya 180 zimeunganishwa na Mifumo zaidi ya 200 inawasiliana na kubadilishana taarifa. Aidha, e-GA inaendelea na mkakati wa kuzihamasisha taasisi za umma kujiunga na Mfumo huo.




Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) (katikati) akifuatilia video ya uzinduzi wa Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa na Mfumo wa Faida Fund mara baada ya Kuzindua mifumo hiyo wakati wa kilele cha Wiki ya Utumishi wa Umma katika viwanja vya Chinangali jijini Dodoma

## NUKUU ZA WAZIRI MKUU

1. Azitaka Taasisi zote za Umma kujiunga na Mfumo huo ifikapo Julai 30, 2025.
2. Asisitiza kuwa, ni lazima taasisi zote kutekeleza maelekezo ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
3. Afurahishwa na faida za Mfumo kwa Serikali

# e-Mrejesho V2 yaipeperusha Tanzania Kimataifa

### Yaingia Fainali Tuzo za WSIS 2025

Na Catherine Peter

Tanzania kupitia Mfumo wa e-Mrejesho toleo la pili (e-Mrejesho V2), imefanikiwa kuingia fainali ya tuzo za Mkutano wa Dunia wa Jumuiya ya TEHAMA mwaka 2025 (World Summit on the Information Society -WSIS 2025 Grand Winner) katika kipengele cha Serikali Mtandao.

Tuzo hizo ambazo huratibiwa na Shirika la Mawasiliano la Umoja wa Mataifa (International Telecommunications Union – ITU), zinalenga kutambua na kuchochea miradi bunifu inayotumia TEHAMA katika kuchangia maendeleo endelevu duniani.


Akieleza kuhusu hatua hiyo, Meneja Mawasiliano wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Subira Kaswaga, amesema kuwa, Mfumo wa e-Mrejesho toleo la pili (V2), umefanikiwa kuingia fainali ya tuzo hio katikae kipengele cha Serikali Mtandao (e-Government AL C7., kati ya mifumo 360 ya TEHAMA iliyofuzu hatua ya awali ya mchujo kutoka zaidi ya maombi 1000 ya mifumo ya kidijiti yaliyowasilishwa kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Meneja huyo amesema, e-GA ilipokea taarifa ya ushiriki wa tuzo hizomwishoni mwa mwezi Aprili, 2025 na kuwahamasisha wananchi kushiriki kwa kupiga kura kwa wingi ili tuzo iweze kuja nyumbani Tanzania.

Aidha, amebainisha kuwa, taarifa ya uthibitisho wa e-GA kuingia hatua ya fainali imepokewa hivi karibunia kutoka ITU kupitia baruapepe na kuwa, washindi wa tuzo hiyo watatangazwa rasmi kwenye Hafla ya Tuzo za WSIS 2025, itakayofanyika wakati wa Tukio la Ngazi ya Juu la Jukwaa la WSIS+20 (WSIS+20 Forum High-Level Event), mjini Geneva kuanzia tarehe 7 hadi 11 Julai, 2025.

Mfumo wa e-Mrejesho (V2) umesanifiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na kusimamiwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ukiwa umeboreshwa kwa kutumia teknolojia ya Akili Mnemba (Artificial Intelligence) katika kukusanya maoni ya wananchi na kuisaidia Serikali kufanya maamuzi.

Mfumo huu unapatikana kwa njia tatu ambazo ni;- kupitia simu ya mkononi kwa kubofya ***152*00#** na kisha kuchagua namba 8 na kisha **namba 2** na kisha fuata maelekezo; kupitia simu janja kwa kupakua **Aplikesheni tumizi** (Mobile App) ya e-Mrejesho inayopatikana kwenye 'Play Store na Apps Store'; na kwa njia ya Tovuti kupitia https://emrejesho.gov.go.tz.






"Nifuraha kubwa kuona wananchi wameweza kuitikia wito na kuwa wazalendo kwa kufanya kazi kubwa ya kuhakikisha wanapiga kura kwa wingi na hatimaye tumefanikiwa kuingia hatua ya fainali, kwa niaba ya Menejimenti ya e-GA tunawashukuru sana"

**Bi. Subira Kaswaga**
Meneja Mawasiliano e-GA

# Hoja za TEHAMA Ripoti ya CAG Zifanyiwe Kazi : Mhandisi Ndomba



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Mhandisi Benedict Ndomba.

**Na Queenter Mawinda**

Wakuu wa Vitengo vya TEHAMA Serikalini, wametakiwa kuzifanyia kazi hoja mbalimbali zinazoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu mifumo ya TEHAMA ili kuhakiksha hoja hizo hazijirudii.

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict Ndomba, wakati wa mafunzo ya siku tatu ya Wakuu wa Vitengo vya TEHAMA kutoka ofisi za Makatibu Tawala Mikoa ya Tanzania Bara na Halmashauri zote nchini.

Amesema kuwa, yapo maeneo ambayo CAG ameyagusa na kuyatangaza katika ripoti ya Ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA hivyo ni jukumu la Wakuu wa Vitengo vya TEHAMA Serikalini, kuhakikisha wanazipitia na kuzifanyia kazi hoja zote zinazowagusa ili zisijirudie.

Sambamba na hilo, Ndomba amewataka viongozi hao kuhakikisha kila mtumishi wa umma katika taasisi husika anakuwa na baruapepe ya serikali, ili awezeshwe kuifikia mifumo mbalimbali ya Serikali.

“Kuna mifumo ya kiutendaji ambayo inamlazimu mtumishi wa umma kuwa na baruapepe ya Serikali ili aweze kuitumia mifumo hiyo, ukiwemo mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office), hivyo ni muhimu kuhakikisha watumishi wote katika taasisi zenu wanazo baruapepe za serikali ili waweze kutekeleza majukumu yao,” amesema Ndomba.

Mafunzo hayo ya siku nne yalifanyika katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Dodoma mwezi April mwaka huu na kuratibiwa na e-GA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, UTUMISHI pamoja na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mafunzo hayo, yalilenga kuwajengea uwezo Wakuu wa vitengo vya TEHAMA kutoka ofisi za Makatibu Tawala Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara na wengine kutoka Halmashauri mbalimbali nchini, katika maeneo ya Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao.

> Nia kubwa ya kufanya hivi ni kuhakikisha tunaboresha utendaji kazi wetu, na kuhakikisha mifumo ya TEHAMA tunayoianzisha au kuisimamia inakidhi matarajio ya serikali katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi

Mhandisi Benedict Ndomba
Mkurugenzi Mkuu e-GA

# Simbachawene Aipongeza Bodi ya Wakurugenzi e-GA

Na Ben Bago

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (Mb), ameipongeza Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa usimamizi mzuri wa taasisi hiyo.

Mhe. Waziri ameyasema hayo Mei 20, mwaka huu wakati alipofanya kikao kazi maalum na Bodi hiyo katika ofisi za e-GA Mtumba jijini Dodoma. Aliongeza kuwa, usimamizi makini wa Bodi hiyo umeiwezesha e-GA kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kufikia malengo iliyojiwekea kwa wakati.

Ameyataja baadhi ya mafanikio hayo kuwa ni pamoja na ujenzi wa mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (Governement Enterprise Service Bus - GovESB), ambao unaziunganisha na kuziwezesha taasisi za umma kubadilishana taarifa kidijitali.

"Moja ya mafanikio ya Bodi hii ni kusimamia utekelezaji wa agizo la Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, la kuhakikisha mifumo ya Serikali inawasiliana na kubadilishana taarifa na hili mmelitekeleza kwa kuhakikisha e-GA inajenga mfumo huu wa GovESB," alisema Waziri.

Alitaja mafanikio mengine kuwa ni pamoja na usimamizi wa miundombinu na mifumo ya TEHAMA Serikalini, sambamba na kuimarisha na kudhibiti usalama wa mifumo hiyo.

Waziri alisema, umakini wa bodi hiyo umeiwezesha e-GA kusimamia usalama wa mifumo ya TEHAMA Serikalini jambo ambalo lisingesimamiwa vizuri lingeweza kuleta hatari za kiusalama.

Aliongeza kuwa, usimamizi makini wa Bodi na menejimenti ya e-GA umekuwa chachu katika mageuzi ya Serikali Mtandao, na kuipa nchi heshima kubwa katika anga za kimataifa ikiwemo kupokea tuzo mbalimbali.

"Mwaka 2024 tulishinda tuzo ya Umoja wa Mataifa ya Utoaji wa Huduma kwa Umma (UN Public Service Innovation Award) kupitia mfumo wa e-Mrejesho na mwaka huu tumeingia tena katika mashindano ya Tuzo za Dunia za Jumuiya za TEHAMA (World Summit on The Information Society - WSIS), tumechaguliwa kushiriki katika ushindani wa tuzo hizo," alisema Mhe. Waziri.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya e-GA Dkt. Mussa Kissaka, alimshukuru Mhe. Waziri kwa pongezi na kuahidi kuendelea kuisimamia vizuri e-GA ili iweze kufikia malengo yake.

"Bodi ya wakurugenzi inaahidi kuendelea kuisimamia vizuri e-GA, licha ya mafanikio haya ambayo Mhe. Waziri umeyataja hapa leo, tutaendelea kuisimamia vizuri zaidi e-GA na kuhakikisha inatekeleza majukumu yake na kuendelea kushinda tuzo za kimataifa," alisema Dkt. Kissaka.

Pamoja na hayo, Dk. Kissaka aliishukuru Menejimenti ya e-GA kwa ushirikiano inaoupata kwakuwa hutekeleza maelekezo yote yanayotolewa na bodi hiyo kwa wakati.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (Mb) akizungumza na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao



Bi. Joan Valentine

# Wachambuzi wa Mifumo waaswa Kuongeza Weledi na Ufanisi

Na Ben Bago

Wachambuzi wa Mifumo ya TEHAMA wa Taasisi za Umma, wameaswa kuongeza weledi na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuepuka makosa yanayoweza kuisababishia hasara Serikali.

Rai hiyo imetolewa Aprili 18, mwaka huu na Afisa TEHAMA Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Joan Valentine wakati wa kuhitimisha mafunzo maalum ya siku tano (05) kwa Wachambuzi wa Mifumo ya TEHAMA (Certified Business Analysis Professional) yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.

Alisema kuwa, katika hatua za awali za ukusanyaji wa mahitaji ya miradi ya TEHAMA, wataalamu hao wanapaswa kuzingatia weledi na umakini, ili kutengeneza mifumo ya TEHAMA itakayoweza kutatua changamoto zilizopo, na kuiwezesha serikali kutoa huduma bora kwa wananchi.

Alibainisha kuwa, Serikali inawekeza rasilimali nyingi katika utekelezaji wa miradi ya TEHAMA kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, hivyo ni wajibu wa kila mtaalamu kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa ufanisi ili kuleta tija iliyokusudiwa.

**“Makosa madogo katika hatua za awali za miradi ya TEHAMA yanaweza kuathiri utekelezaji mzima wa mradi na kuleta hasara kwa Serikali, hivyo sisi wataalamu tunaoshiriki katika hatua za awali za ukusanyaji wa mahitaji, ni muhimu tuzingatie weledi na uadilifu,”**

**Bi. Joan Valentine**
Afisa TEHAMA Mkuu

Alifafanua kuwa, wachambuzi wa mifumo ya TEHAMA wanayo nafasi kubwa ya kuzisaidia taasisi za umma kuondoa kasoro mbalimbali za mifumo ya TEHAMA ya taasisi katika hatua za mwanzo za ujenzi wa mifumo hiyo.

“Wajenzi wa Mifumo ya TEHAMA (Developers of ICT systems), hujenga mifumo kutokana na mahitaji yaliyochakatwa na Wachambuzi wa Mifumo, hivyo ikiwa Wachambuzi hao watafanya kazi zao kwa weledi na umakini zaidi, watasaidia kuondoa dosari katika mifumo,” alifafanua Bi. Joan.

Aliongeza kuwa, mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo Wachambuzi wa Mifumo ya TEHAMA katika kuchambua mahitaji ya watumiaji wa mifumo na kuandaa nyaraka sahihi za miradi ya TEHAMA kabla ya utekelezaji wake.

Mchambuzi Mkuu wa Mifumo ya TEHAMA kutoka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi Bi. Kissa Tuntufye, ameishukuru e-GA kwa kuratibu mafunzo hayo kwani yamewaongezea ujuzi katika utekelezaji majukumu yao ya kila siku, wakiwa kama daraja kati ya Wajenzi wa Mifumo na watumiaji wa mifumi ya TEHAMA.

"Ni muhimu kupata mafunzo kama haya ambayo yanatuongezea maarifa ya namna bora ya kuangalia changamoto na kuja na ufumbuzi ambao, tukiwapelekea Wajenzi wa mifumo, watajenga mifumo bora ya TEHAMA na kurahisisha utoaji wa huduma za Serikali kidijitali," alisema Bi. Kissa.

Naye Bi. Leah Makuya, ambaye ni Mchambuzi wa Mifumo ya TEHAMA kutoka Wizara ya Fedha alisema, mafunzo hayo yatachangia katika maendeleo ya Serikali Mtandao kwa kuhakikisha kwamba mifumo inayotengenezwa inatoa majibu kwa changamoto zinazowakabili wananchi.

"Kupitia mafunzo haya, tumepata fursa ya kujifunza mbinu bora za uchambuzi wa biashara (business analysis) na namna ya kuepuka makosa ya kiufundi, ambayo yanaweza kusababisha ucheleweshaji au upotevu wa rasilimali za Serikali kwenye Miradi ya TEHAMA," alisema Bi. Leah.

Mafunzo hayo yalitolewa na kampuni ya kimataifa ya Koenig Solutions ya nchini India, chini ya uratibu wa e-GA, yalihudhuriwa na washiriki kutoka katika taasisi mbalimbali za umma zikiwemo e-GA, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Wizara ya Ardhi, Wizara ya Fedha, pamoja na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Utoaji wa mafunzo hayo ni sehemu ya mikakati ya e-GA ya kuwajengea uwezo wataalamu wa TEHAMA Serikalini, ili kuwa na ujuzi wa kisasa zaidi kadri mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanavyojitokeza kwa kuzingatia sheria zilizopo.






Baadhi ya Wachambuzi wa Mifumo ya TEHAMA kutoka Taasisi mbalimbali wakifuatilia mafunzo maalum ya Uchambuzi wa Mifumo ya TEHAMA (Certified Business Analysis Professional) .




# Maafisa Habari Watakiwa Kulinda Taarifa za Serikali

Na Mussa Enock

Maafisa Habari, Uhusiano na Mawasiliano wa Serikali, wametakiwa kutumia mifumo rasmi ya Serikali katika mawasiliano ya kikazi ili kulinda taarifa za Serikali dhidi ya vitendo vya uhalifu mtandaoni.

Wito huo umetolewa April mwaka huu na Mkurugenzi wa Huduma za TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw. Ricco Boma, wakati akichangia mada kuhusu mabadiliko ya teknolojia katika mawasiliano, kwenye Mkutano Mkuu wa mwaka wa Chama cha Maafisa Habari, Uhusiano na Mawasiliano wa Serikali (TAGCO) uliofanyika mkoani Morogoro.

Alisema kuwa, katika ulimwengu wa sasa taarifa ni hazina muhimu inayopaswa kulindwa hhivyo, Maafisa Habari, ambao ndio wenye jukumu la kuuhabarisha umma kuhusu masuala mbalimbali yanayozihusu taasisi zao, wanapaswa kulinda taarifa za Serikali kwa kutumia mifumo rasmi ya Serikali katika Mawasiliano yao.
Alibainisha kuwa, ikiwa Maafisa hao watatumia mifumo isiyo rasmi katika mawasiliano yao, wanaweza kuhatarisha baadhi ya taarifa za Serikali kuwafikia wasiohusika, na hivyo kuliweka taifa katika hatari za kiusalama katika maeneo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Aidha, aliongeza kuwa, matumizi ya TEHAMA katika mawasiliano yana faida nyingi, ikiwa ni pamoja na habari kuwafikia wananchi kwa wakati, lakini pia yanaweza kuleta athari ikiwa mawasiliano ya taarifa za serikali yatafanyika kupitia mifumo isiyokuwa rasmi.

Aliitaja mifumo mingine kuwa ni pamoja na Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office) na Mfumo wa e-Mrejesho unaowawezesha wananchi kutoa maoni, ushauri, malalamiko au pongezi kwa Serikali na kisha kupata mrejesho kwa wakati.

**“Tunayo mifumo mbalimbali kwa ajili ya mawasiliano Serikalini, kama vile Mfumo wa baruapepe Serikalini (GMS), hivyo ni lazima tuhakikishe kuwa, mawasiliano yote ya kiofisi tunayafanya kupitia Mfumo huu na si baruapepe binafsi ili kuhakikisha usalama wa taarifa zetu.”**

**Bw. Ricco Boma**
Mkurugenzi wa Huduma za TEHAMA



Mkurugenzi wa Huduma za TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw. Ricco Boma .

# Wanawake Wapo Katika Hatari Zaidi Ya Kupata Uchakavu Wa Mifupa



Daktari Bingwa Idara ya Upasuaji wa Mifupa na Mfumo wa Fahamu katika Hospitali ya Benjamin Mkapa Dkt. Fanuel Bellet .

Na Queenter Mawinda

Kama wewe ni mwanamke wa zaidi ya miaka 30 basi ni vyema kuzingatia mwenendo wa maisha yako ili kuepukana na magonjwa nyemelezi yanayoweza kuambatana na umri, ikiwemo uchakavu wa mifupa.

Uchakavu wa mifupa ni ugonjwa unaombatana na vichochezi vikuu viwili; Mosi ni sababu za kibaiolojia, ambazo huambatana na umri, na sababu ya pili ni mfumo mzima wa maisha ya mtu binafsi.


Daktari Bingwa Idara ya Upasuaji wa Mifupa na Mfumo wa Fahamu katika Hospitali ya Benjamin Mkapa Dkt. Fanuel Bellet ameeleza kuwa, katika mwili wa mwanadamu kuna seli aina mbili; seli zinazojenga mifupa kitaalamu zinaitwa 'osteoblast', na seli zinazopunguza au kuondoa mifupa inayozidi lile umbo maalum la mfupa husika ambapo kitaalamu zinaitwa 'osteoclast'. Seli hizi mbili hupokezana kazi wakati wa ujenzi wa mifupa.

Kadiri umri unavyozidi kwenda, mabadiliko ya hatua ndogo ndogo yanatokea katika seli za mwili kila siku. Mabadiliko hayo huanza kujitokeza katika viungo vyote vya mwili, ikiwemo mifupa ambayo nayo huendelea kuchakaa kadiri umri unavyokwenda.

Inapofika miaka 30, seli zinazohusika na kutengeneza mifupa yani 'osteoblast' zinapunguza uwezo wa kutengeneza mifupa, na kupelekea seli zinazopunguza mifupa osteoclast kuanza kufanya kazi yake. Seli hizi za kupunguza mifupa hufanya kazi yake ya kufanya usafi au kutoa mifupa iliyozidi kwa kushirikiana na seli zingine zinazoitwa Osteocytes.

Katika miaka ya mwanzo yaani (miaka 0 hadi 30), seli zinazojenga mifupa zinakuwa nyingi kuliko zinazo ondoa au kusafisha mifupa.

Baada ya hapo, seli zinazojenga zinaanza kupungua idadi taratibu na kuzidiwa na zile zinaoondoa au kusafisha mifupa. Katika hatua hii endapo mtu hatazingatia mazoezi na vyakula sahihi vya kuimarisha mifupa, basi anaweza kupata uchakavu wa mifupa.





Daktari Bingwa Idara ya Upasuaji wa Mifupa na Mfumo wa Fahamu katika Hospitali ya Benjamin Mkapa Dkt. Fanuel Bellet akionesha picha ya Mfumo wa Mifupa ya Mwanadamu

## Mifupa

Inakadiriwa kuwa binadamu ana idadi ya mifupa inayofikia 206. Mifupa ya mwili mzima wa mwanadamu inaanza kutengenezwa tumboni mimba inapokuwa na wiki sita au saba tangu itungwe na huendelea kutengenezwa kwa kurefuka na kupanuka kadiri anavyokua kiumri hadi miaka 30.

## Kwanini wanawake wapo katika hatari zaidi?

"Wanawake wametajwa kuwa kwenye hatari zaidi ya kupata ugonjwa huu kutokana na kupungua kwa hormone ya ostrogen na hivyo kukoma hedhi yaani kupata 'menopause' mapema, hali inayopelekea mifupa kuchoka haraka", amesema Dk. Bellet.

Sababu nyingine imetajwa kuwa ni ukosefu wa mazoezi. Ipo tofauti kubwa miongoni mwetu kutokana na aina ya maisha ya kila mmoja. Utofauti huo wa maisha, huonesha kuwa na athari tofauti kwa kila mtu kutokana na sababu mbalimbali zinazoweza kuathiri afya ya mifupa. "Kundi la wanawake wengi si wapenzi wa kufanya mazoezi mara kwa mara. Hali hii inapelekea kuwa na uzito mkubwa na hivyo mifupa kuchoka haraka zaidi kuliko wanaume", amefafanua Dkt. Bellet.

Dkt. Bellet ameeleza kuwa, kadiri mifupa yetu inavyobeba uzito au kufanyishwa mazoezi mara kwa mara ndivyo inavyoimarika. Uzito huo ni pale mtu anapotembea, anapokimbia au kubeba vitu vyenye uzito fulani. Vyote kwa pamoja huimarisha mifupa na misuli lakini ukosefu wa hayo hufanya mifupa kuwa dhaifu.

## Chanzo cha Uchakavu wa Mifupa nini?

Kwa mujibu wa Dkt. Bellet asilimia 60-70 ya wagonjwa hukabiliwa na matatizo ya uti wa mgongo na asilimia 20-30 ya wagonjwa wanakabiliwa na matatizo ya nyonga na magoti, huku wanawake wa kuanzia umri wa miaka 40 wakiwa kwenye hatari zaidi ya magonjwa haya, na wanaume wa umri kuanzia miaka 50 wakitajwa kuwa kwenye kundi hili la wahanga.

Sababu zinazopelekea uchakavu wa mifupa zimetajwa kuwa ni pamoja na;

1. Uzito mkubwa
2. Mabadiliko ya Umri
3. Ukosefu wa mazoezi
4. Matumizi ya baadhi ya dawa kama vile dawa zinazopunguza kinga ya mwili
5. Upungufu wa virutubisho vinavyoimarisha mifupa kama vile kalsiamu, vitamini D, fosforasi na madini ya sodiumu
6. Upungufu wa vyakula vyenye protini kama vile samaki, nyama, maziwa, maharage
7. Matumizi ya vinywaji kama soda aina coke, pombe, sigara vinapunguza ubora wa mifupa.

## Viashiria na matibabu

Mgonjwa mwenye uchakavu wa mifupa, atakuwa na maumivu ya mifupa yatakayopelekea kushindwa kutembea. Hivyo Dkt. Bellet amesema, mgonjwa akiwa katika hali hii hupewa dawa zitakazosaidia kutuliza hali au maumivu hayo na kushauriwa kufanya mazoezi maalumu yanayotolewa hospitali na wataalamu wa mifupa (Physiotherapy).

Lakini endapo hali hii itazidi na kufanya hali ya mgonjwa kuwa mbaya zaidi, basi mgonjwa hufanyiwa upasuaji wa kubadilisha goti au nyonga.

## Mafanikio ya matibabu

Hadi sasa wagonjwa zaidi ya 200 wamefanyiwa matibabu ya mifupa katika Hospitali ya Benjamini Mkapa kwa mafanikio. Huku malengo yakiwa ni kuongeza zaidi idadi ya wagonjwa watakaotibiwa kwa mafanikio.

## Nini kifanyike?

Dkt. Bellet amesema ni vema wananchi wafahamu kuwa, mifupa inabadilika kutokana na umri, ukosefu wa mazoezi lakini pia ulaji wa aina fulani ya vyakula hasa vilivyosindikwa viwandani. Kwa kuzingatia hilo, amewasihi wananchi kuzingatia ushauri wa kitaalamu na kujua mwenendo wa afya zao kwa kufanya uchunguzi wa mara kwa mara wa afya, ili kubaini viashiria vya magonjwa ya mifupa mapema na kuanza matibabu.




Mwandishi wa makala hii Bi. Queenter Mawinda (Kulia) akipokea zawadi ya kitabu cha Afya ya Uti wa Mgongo kutoka kwa mtunzi wa kitabu hicho Dkt. Fanuel Bellet ambaye pia ni Daktari Bingwa Idara ya Upasuaji wa Mifupa na Mfumo wa Fahamu katika Hospitali ya Benjamin Mkapa.

# Herieti Daudi : Ndoto Hai Katika Kesho ya TEHAMA




"Kupitia Akili Mnemba (AI) tunaweza kutatua changamoto mbalimbali zilizopo kwenye jamii yetu ikiwemo uchafuzi wa mazingira.Tunaweza kupata ufumbuzi wa changamoto hizi kidigiti na kuwa na jamii yenye mazingira safi kwa afya zetu na mazingira yanayotuzunguka."

**Herieti Daudi**
**Mwanafunzi**

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Jerry William Silaa akimkabidhi tuzo mwanafunzi Herieth Daudi

**Na Ben Bago**

KATIKA kijiji kidogo cha Kinampanda, Wilaya ya Iramba mkoani Singida, anapatikana msichana mdogo mwenye ndoto kubwa na ari isiyozimika katika uwanja wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Huyu ni Herieti Daudi, mwanafunzi wa kidato cha tatu (3) katika shule ya Sekondari Tumaini wilayani Iramba, amejitokeza kuwa mfano wa kuigwa kwa wasichana wengi katika shule hiyo wakivutiwa na mapenzi yake makubwa katika TEHAMA akiwa na ndoto ya ubobevu katika teknolojia ya Akili Mnemba - **(Arificial Intelligence–AI**

"Matarajio yangu makubwa ni kuwa Mhandisi mbobezi katika eneo la AI, napenda kuwa miongoni mwa watanzania wanaochochea maendeleo ya TEHAMA na kuhamasisha vijana wengi hasa wa kike kupenda tasnia hii," ameeleza Herieti.

Herieti anasema, alipata shauku ya kupenda teknolojia baada ya kupata nafasi ya kuchaguliwa kujiunga na mradi maalum wa Wasichana katika TEHAMA (Girls in ICT) unaondeshwa na serikali ya Tanzania kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote - (UCSAF).

Katika mradi huo, Herieti alichaguliwa kuwa miongoni mwa washindi sita (6) wa kitaifa, huku akiibuka mshindi kwa wanafunzi kutoka kanda ya kati inayojumuisha mikoa ya Dodoma, Singida na Tabora.

Ndoto kubwa ya Heriet ni kujifunza zaidi na kuwa mbobezi katika TEHAMA, hasa katika eneo la AI ambalo anaamini kuwa litaweza kuleta mabadiliko chanya katika sekta mbalimbali nchini.

Dhamira yake ni kujiendeleza na kutumia ujuzi wake kuunda suluhisho za kiteknolojia zitakazosaidia jamii yake na taifa kwa ujumla, ikiwemo kuunda programu inayoweza kusaidia jamii katika kukusanya taka kidigitali.

Licha ya changamoto mbalimbali, ikiwa ni pamoja na upatikanaji mdogo wa vifaa vya TEHAMA na mtandao wa intaneti katika maeneo ya vijijini, Herieti ameendelea kuwa na ari na bidii katika kujifunza ili kufikia malengo yake.

"Wito wangu kwa Serikali ni kuendelea na jitihada za kuwafikia wasichana wengi zaidi katika sekta ya TEHAMA, iendelee kuwekeza hususani katika maeneo ya vijijini ili kusaidia kuibua vipaji mbalimbali vitakavyosaidia Taifa katika eneo hili," ameshauri Herieti.

Herieti ni mfano halisi wa jinsi ambavyo wasichana wanaweza kung'ara katika nyanja za TEHAMA ikiwa watapewa fursa na msaada unaohitajika ili kutimiza ndoto zao.

Herieti anaamini kwamba, kupitia jitihada hizo za serikali na wadau wengine,TEHAMA itaendelea kuwa chachu katika kuleta mabadiliko katika jamii na taifa kwa ujumla.

“Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imekuwa na mchango mkubwa katika uendeshaji wa Halmashauri zetu. Kupitia huduma za ushauri na uelekezi tunazozipata kutoka e-GA, tumeweza kuboresha huduma tunazotoa kwa wananchi kupitia mifumo mbalimbali ya TEHAMA,

**Edward Selestine Rumanyika**
**Mkuu wa kitengo cha TEHAMA- Urambo**






Tunaipongeza Serikali kwa kutujali wananchi wa vijijini, huku wengi wetu tunatumia simu ndogo ambazo hazina hata mtandao, lakini kupitia *152*00# tunaweza kupata huduma na taarifa mbambali za serikali. Mimi napata huduma zote za Serikali kwa njia ya mtandao.

**Pater Karumbi**
**Mkazi wa Lukole, Mpwapwa**

Tunalipongeza sana Dawati la Msaada wa Kiufundi (HelpDesk) la e-GA kwa kuwa karibu na taasisi za Umma kwani ukiwasiliana nao hawaishii tu kukusikiliza na kukupa suluhisho la changamoto yako bali pia wanakufuatilia kujua mwisho wake, hivyo hata kama ukitingwa na mambo mengi wanakukumbusha ili kupata mrejesho wa utatuzi wa changamoto yako kama imekwisha

**Magreth Vicent Mtenga**
**AfisaTEHAMA Manispaa ya Moshi**






Tunaipongeza Serikali kwa kutengeneza mfumo huu wa eMrejesho, zamani waliweka vile viboksi vya maoni watu waliweka maoni lakini hayakuwa yakijibiwa na wananchi hawakujua namna ya kupata mrejesho. Lakini kwa kupitia mfumo huu (eMrejesho) kila kitu kimekuwa rahisi sana. Mfumo huu una faida kubwa ikiwemo kupunguza gharama za wananchi kufuatilia changamoto zao kutoka katika Taasisi za Umma

**Gilbet Koronko**
**AfisaTEHAMA Manispaa ya Moshi**

# "Gas Monitoring System" Mfumo wa Kufuatilia Kiwango cha Gesi Kidijitali




**Na Ben Bago**

Matumizi ya nishati safi ya gesi ya kupikia yanazidi kuimarika siku hadi siku. Kuongezeka kwa matumizi haya, kumekiibua Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (e-Government Research, Innovation and Development Centre - **eGOVRIDC**), kufanya ubunifu kwa kutengeneza mfumo wa ufuatiliaji wa gesi kidijitali.

Mfumo huu ujulikanao kama 'Gas Monitoring System', ambao kwa sasa upo katika hatua za majaribio, unalenga kuwawezesha watumiaji kutambua kiasi cha gesi kilichobaki baada au wakati wa matumizi.

Kupitia mfumo huu, watumiaji wataweza kufuatilia kiwango cha gesi kilichopo kwa wakati, hata wanapokuwa mbali na makazi yao. Aidha, mfumo huu unatarajiwa kuwa suluhisho la kadhia inayowapata watumiaji wa gesi za kupikia majumbani, pale nishati hiyo inapoisha ghafla, bila ya mtumiaji kuwa na taarifa.

Jinsi Mfumo unavyofanya kazi

Mfumo huu unafanya kazi kwa kutumia teknolojia ya 'Internet of Things- IoT', ambapo kifaa maalum kimebuniwa ili kupima kiasi cha gesi kilichopo kwenye mtungi, na kuwasilisha taarifa hizo kwa mtumiaji kupitia aplikesheni tumizi, atakayoiweka kwenye simu yake ya mkononi.

Aidha, mfumo huu umejengwa kwa kutumia kifaa cha kielektroni, ambacho kimeunganishwa na **'sensor'** maalum za ultrasonic. Sensor hizi hufanya kazi kwa kutuma mawimbi ya sauti kupitia kuta za mtungi wa gesi, ili kuweza kupima kiwango cha gesi kilichopo.

Mawimbi ya sauti yanaporejea kwenye kifaa, data hii inakusanywa na kuhifadhiwa, kisha taarifa hizo zinachakatwa na 'microcontroller' ili kubaini asilimia halisi ya gesi iliyobaki kwenye mtungi.

Mara baada ya kuchakata taarifa, mfumo hutuma data hiyo kwenye '**cloud server**' kwa njia ya **Wi-Fi,** watumiaji wanaweza kuona asilimia ya gesi iliyobaki kwa kutumia aplikesheni tumizi ya simu (mobile app), au tovuti, huku wakipata taarifa za kila baada ya matumizi.

Vilevile, mfumo unatoa onyo la tahadhari **'warning'** pale gesi inapokaribia kuisha, kupitia ujumbe mfupi (SMS), taarifa hizi za tahadhari ni muhimu katika kusaidia watumiaji kupanga matumizi yao ya gesi, huku wakifahamu ni wakati gani watapaswa kujaza gesi.

## Faida za mfumo huu

Mfumo wa 'Gas Monitoring System' unawawezesha watumiaji kufuatilia kiwango cha gesi kwa wakati, na kufahamu kiasi cha gesi kilichopo, hivyo kuweza kupanga matumizi yao ipasavyo.

Mfumo unaweza kutoa tahadhari '**alert'** ya gesi inapokaribia kuisha kuwa kutuma ujumbe mfupi kwa mtumiaji na hivyo kuweza kupanga mipango yake mapema. Aidha, ufikiaji wa data mahali popote ni faida nyingine muhimu, taarifa zinazohifadhiwa kwenye **'cloud server',** zinawapa watumiaji fursa ya kuzifikia wakati wowote na mahali popote hasa wanapokuwa mbali na nyumba zao.

Kwa kutumia aplikesheni tumizi ya simu au tovuti, mtumiaji ataweza kupata taarifa muhimu na kufanya maamuzi kwa wakati ikiwemo kuandaa fedha kwa ajili ya ununuzi wa gesi.

Mfumo huu ni rahisi na rafiki kutumia kwani haimlazimu mtumiaji kuwa na ujuzi wa kiufundi. Aidha, programu ya simu inatoa mwongozo mzuri wa matumizi, hivyo hata wale wenye uelewa mdogo wa teknolojia wanaweza kuitumia bila kikwazo.

Katika suala la kiuchumi, mfumo huu unaweza kuwasaidia wafanyabiashara wadogo na wa kati kupunguza hasara zinazoweza jitokeza pale ambapo gesi huisha ghafla.



# e-GA ilivyotekeleza Ilani ya CCM 2020 – 2025

**Na Catherine Peter**

Miaka mitano sasa inatimia tangu Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ianze rasmi utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020–2025 katika eneo la ujenzi wa Serikali Mtandao .

Katika kipindi hiki, e-GA imekuwa kinara katika kuongoza mageuzi ya utendaji wa Serikali kupitia TEHAMA ili kuboresha utendaji kazi katika taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa umma, zikiwa zinapatikana kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu.

Utekelezaji wa Mikakati thabiti ya Ilani ya CCM kwa kipindi hiki cha miaka mitano (chini ya Serikali ya Awamu ya Siti inayoongiozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan), kwa kuwekeza kwenye TEHAMA, ndiko kumeiwezesha e-GA kufikia malengo ya utekelezaji wa Ilani hiyo.

Kupitia Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019, e-GA imepewa mamlaka ya kusimamia, kuratibu na kukuza jitihada za Serikali Mtandao Pia, e-GA inawajibika kuitekeleza Ilani ya chama kilichopo madarakani katika eneo la Serikali Mtandao.

Ilani ya CCM ya 2020 - 2025, imebainisha maeneo muhimu ya kipaumbele katika ujenzi wa Serikali Mtandao kuwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya TEHAMA, upanuzi wa mtandao wa intaneti serikalini, huduma za serikali kwa njia ya simu (mGov), vituo vya kuhifadhi taarifa (Data Centers), na mifumo ya kidijitali inayowezesha utendaji bora wa serikali.

Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba amebainisha kuwa, utekelezaji wa Ilani ya CCM tangu mwaka 2020 – 2025 umeleta mageuzi chanya ya matumizi ya TEHAMA Serikalini na kuchochea ukuaji wa uchumi wa kidijiti.

Amebainisha kuwa, moja ya kipaumbele cha Ilani hiyo ni kuimarisha Serikali Mtandao kwa kuboresha ujenzi na upanuzi wa miundombinu shirikishi ya TEHAMA, ambapo e-GA imefanikiwa kujenga na kusimamia mtandao wa mawasiliano Serikalini (Government Communication Network - GovNet) na kuunganisha taasisi za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

“Kwanza tumeweza kujenga na kusimamia miundombinu shiririkishi ambayo hutumiwa na taasisi zote za umma, lakini pia tumekuwa na uhakika wa upatikanaji wa intaneti, na uwezo wa kufatilia na kubaini ikiwa kuna changamoto mahali na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za Serikali wakati wote kwakuwa sisi ndio tunaosimamia miundombinu hii”, amesema Ndomba.

Ameeleza kuwa, mifumo shirikishi ni moja ya kipaumbele kilichowekwa na ilani ya CCM 2020-2025, ambapo e-GA imefanikiwa kujenga mifumo shirikishi inayotumika katika taasisi za umma ikiwemo Mfumo wa baruapepe Serikalini (Government Mailing System), Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office), Mfumo wa

Usimamizi wa Shughuli za Taasisi (Enterprise Resource Management Suite), Mfumo wa kuomba vibali vya kusafiri nje ya nchi kwa watumishi wa Umma wa e-Vibali, na Mfumo wa Huduma za Serikali kwa njia ya simu ya mkononi (M-Gov).

Ndomba ameeleza kuwa, mifumo hii hutumiwa na taasisi mbalimbali za umma na hivyo kurahisisha utendaji kazi na kuziwezesha taasisi kufikia malengo kwa wakati kwa kuondoa urasimu, sambamba na kuboresha utoaji wa huduma bora kwa umma.

Pia, e-GA imeshirikiana na taasisi mbalimbali za umma kujenga mifumo shirikishi ya kisekta, ikiwa ni utekelezaji wa ilani ya chama tawala. e-GA kwa Kushirikiana na Ushirika imetengeneza Mfumo wa Vyama vya Ushirika (MUVU) unaowezesha wakulima kufahamu mwenendo wa uuzaji wa mazao yao katika vyama vya USHIRIKA na pia imeshirikiana na Wizara ya Maji kutengeneza Mfumo wa ulipaji wa Ankara za Maji (MAJIIS).

Aidha, e-GA imefanikiwa kujenga Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (Government Enterprise Service Bus), na kuziunganisha taasisi 184, mifumo 221 inayowasiliana na kubadilishana taarifa kwa usalama.

Hii ni hatua kubwa katika kupunguza urudufu wa mifumo na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa umma.

"Uwepo wa vituo vya Serikali vya kuhifadhi mifumo (Government Data Centres) imewezesha Serikali kudhibiti taarifa zake katika mazingira salama ambayo ni hatua muhimu katika kufikia na serikali mtandao yenye tija, bila kuwa na mahali salama pa kuhifadhi taarifa zetu, hatuwezi kuwa na Serikali Mtandao yenye tija," amesema Ndomba.

Ameongeza kuwa, eneo jingine la utekelezaji wa ilani ya CCM ni kuimarisha ulinzi wa mifumo na taarifa za serikali dhidi ya matishio ya usalama wa mtandaoni, kwa kuandaa Mkakati wa Usalama wa Mtandao wa Serikali 2022, kutoa mafunzo ya usalama wa TEHAMA kwa taasisi za umma, kufanya tathmini ya mifumo ya TEHAMA katika taasisi hizo pamoja na kufuatilia usalama wa miundombinu muhimu ya TEHAMA kwa saa 24, siku 7 za wiki.

Ukuaji wa matumizi ya teknolojia mpya nacho ni kipaumbele cha ilani ambapo, e-GA kupitia Kituo chake cha Utafiti na Ubunifu cha Serikali Mtandao (eGovernment Research Innovation and Development Centre -eGOVRIDC), hutoa nafasi kwa vijana wa Kitanzania ya kufanya tafiti na bunifu za teknolojia hizo, ili kutengeneza mifumo itakayorahisisha utoaji wa huduma kwa umma.

"Kupitia kituo hiki, mifumo mbalimbali imetengenezwa na baadhi inatumika katika taasisi za umma ikiwemo mfumo wa uendeshaji vikao kidijitali wa e-Mikutano na Mfumo wa mawasiliano kati ya wananchi na Serikali wa e-Mrejesho," amefafanua Ndomba.

Aidha, e-GA imesaini mikataba ya ushirikiano na vyuo 14 vya Elimu ya Juu kwa ajili ya tafiti na ubunifu wa kidijitali, ili kuendeleza vipaji vya vijana na kuongeza matumizi ya teknolojia mpya.

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, e-GA itaendelea kusimamia utekelezaji wa Ilani ya chama kitakachokuwa madarakani baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025 kupitia sehemu ya ujenzi wa serikali mtandao, ili kuchangia katika kujenga Tanzania ya kidijitali inayotumia teknolojia kwa maendeleo ya watu wake kijamii, kiuchumi, na kiutawala. Na sasa Serikali Mtandao si ndoto tena, ni uhalisia unaoonekana.









# Pongezi



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), akimkabidhi tuzo Bw. Joel Makunja kama shukrani ya kutengeneza Mfumo wa Kubadilishana Taarifa Serikalini (Government Enterprise Service Bus - GovESB) katika kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka 2025.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), akimkabidhi tuzo Bw. Salum Mohamed kama shukrani ya kutengeneza Mfumo wa Kubadilishana Taarifa Serikalini (Government Enterprise Service Bus - GovESB) katika kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka 2025.

# Maonesho




Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry William Silaa (Wa pili kulia)) ,akipokea maelezo kutoka kwa Afisa Habari Mwanadamizi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi.Queenter Mawinda, juu ya huduma mbalimbali zitolewazo na Mamlaka, wakati wa Mkutano wa 14 wa jukwaa la Afrika la Utawala wa Mtandao jijini Dar Es Salaam.



Afisa TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw. Frank Alex (Kulia), akielezea kuhusu mifumo na huduma mbalimbali za Mamlaka kwa wananchi waliotembelea banda la e-GA katika Mkutano wa 14 wa jukwaa la Afrika la Utawala wa Mtandao Jijini Dar Es Salaam.

# Maonesho




Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), akizungumza mara baada ya kupewa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya e-GA wakati wa maonesho ya wiki ya Utumishi wa Umma.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (Mb), akisaini Kidijitali wakati aliapotembelea banda la maonesho la Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma.

# Mafunzo



Meneja wa Udhibiti na Viwango vya Serikali Mtandao Bi. Sultana Seiff, akiwasilisha mada wakati wa Mafunzo ya Wakuu wa Vitengo vya TEHAMA wa Mikoa na Halmashauri za Tanzania Bara yaliyofanyika jijini Dodoma. Maafisa hao walijengewa uwezo kuhusu Sheria,Kanuni,Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao



Afisa TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Pulcheria Sumia, akitoa maelezo kuhusu mifumo na bunifu mbalimbali zilizobuniwa na kusanifiwa na e-GA kwa baadhi ya washiriki wa kikao Kazi cha Wakuu wa Vitengo na Idara za TEHAMA wa Taasisi na Mashirika ya Umma.Kikao hicho kilifanyika mwezi Juni jijini Dodoama.

# BODI YA UHARIRI

## MWENYEKITI
Mhandisi Benedict B. Ndomba

Mkurugenzi Mkuu

## WAJUMBE
CPA (T) Salum Mussa

Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji

SACP Hamis Ali

Mkaguzi Mkuu wa Ndani

SACP Rafael Rutaihwa

Meneja wa Huduma za Sheria

Long'ida Oltetiai

Meneja wa Huduma kwa Wateja na Tawimu

## MHARIRI
Subira Kaswaga

Meneja Mawasiliano

## WAANDISHI
Catherine Peter | Afisa Habari Mwandamizi

Queenter Mawinda | Afisa Habari Mwandamizi

## WAPIGA PICHA
Mussa Enock |Afisa Habari

Ben Bago |Afisa Habari

## MSANIFU KURASA
Edger Msamba | Afisa TEHAMA